Association of Women in Tourism Tanzania (AWOTTA)
House No.108/Plot 1334
Haile Selassie Road
Masaki, Dar es Salaam,Tanzania

Mobile: Mobile: +255 622 819 889/ +255 712 748 282/
+255 718 541 751

email: info@awotta.org
website: www.awotta.org

YAH: MWALIKO WA KUSHIRIKI KATIKA MAONYESHO YA KWANZA YA UTALII WA NDANI "UWANDAE EXPO 2019" TAREHE 15-17 FEBRUARI, 2019

Chama cha Wanawake katika Utalii Tanzania (AWOTTA) kwa kushirikiana na Wizara ya Maliasili na Utalii (MNRT), Bodi ya Utalii Tanzania (TTB), Chama cha Wanawake Wafanyabiashara Tanzania (TWCC) na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) inapenda kukufahamisha kuwa inaandaa Maonyesho ya Kwanza ya Utalii wa Ndani "UWANDAE EXPO 2019" yatakayofanyika katika Viwanja vya Makumbusho ya Taifa (National Museum), barabara ya Shaaban Robert, Dar es Salaam. Maonesho yataanza tarehe 15 hadi 17 Februari, 2019. Kauli Mbiu ya Maonyesho haya ni: ***"Tambua ushindani wa Kibiashara katika Utalii wa Ndani Tanzania".***

Maonesho haya yanatarajiwa kufunguliwa rasmi na **Mhe. Dr. Hamisi Kigwangala, Waziri wa Maliasili na Utalii** siku ya Ijumaa tarehe, 15 Februari 2019.

Lengo la Maonyesho haya ni kuanzisha utambuaji wa mapana ya sekta ya Utalii wa Ndani na fursa kubwa za uwekezaji na ajira zinazoambatana na kukua kwa sekta hii muhimu. Maonyesho yatawaunganisha wafanyabiashara wa bidhaa na huduma katika maeneo mbali mbali yanayosababisaha safari za watanzania. Wafanya biashara hawa na vyombo vinavyowezesha uwekezaji, watatumia jukwaa hili kukuza uhusiano baina ya Washiriki na Watembeleaji wa maonesho. Watu elfu tatu wanategemewa kuhudhuria maonyesho.

Faida ya kushiriki:

- Kuonyesha bidhaa au huduma wanazozalisha au wanazotoa;
- Kupata fursa ya kujifunza teknonolija mpya na ujuzi kutoka kwa washiriki wengine;
- Kupata fursa ya kushiriki katika kongamano na semina ya bure itakayofanyika sambamba na maonyesho hayo;
- Kukutana na Wafanyabiashara, Wawekezaji, washauri wa kibiashara na Wasambazaji wa huduma mbalimbali;
- Kupata kutangazwa kwenye utandawazi wa kitaifa na kimataifa kwa njia mbalimbali;
- Kupata fursa mbali mbali ambazo ni pamoja na tiketi ya raffle, vocha ya malazi, zawadi za kusafiri n.k.

Aidha, ni fursa ya kimkakati ya kuwahamasisha wananchi wa Tanzania kupenda kutumia huduma zinazotolewa na wadau wa sekta ya utalii hapa nchini.

Maonyesho haya yanatarajiwa kushirikisha, Wizara, Taasisi, Makampuni pamoja na Wafanyabiashara wa sekta mbalimbali. Sambamba na maonyesho haya, kutakuwa pia na kongamano na semina ya washiriki juu ya "Biashara, Uwekezaji na Ajira katika Uta/ ii wa Ndani ambayo itatolewa bure (idadi ni watu 250 tu kwa siku moja wataruhusiwa, hivyo jiandikishe mapema kabla nafasi hazijaisha).

Gharama za ushiriki ni kama ifuatavyo:-

Daraja	Ukubwa wa Gharama Banda		Vitu unavyopata
Platinum	3x6 sqm	Tshs. 800,000.00 na Ufadhili usiopungua Tshs. 2.5 Milioni	Banda, meza, viti viwili (bora), tiketi 5 za Cocktail ya Ufunguzi wa Maonyesho, nembo kuwekwa kwenye matangazo, kutangaza bidhaa kwenye documentarv
Premium	3x6 sqm	Tshs. 800,000.00	Banda, meza, viti wiwili (bora), tiketi 3 za Cocktail ya Ufunguzi wa Maonyesho
Corporate	3x3 sqm	Tshs. 500,000.00	Banda, meza, viti viwili, tiketi 1 ya Cocktail ya Ufunguzi wa Maonyesho
MSEs	2x3 sqm	Tshs. 300,000.00	Banda, meza na viti viwili (watu wawili wanaweza kutumia banda moja kwa mkataba wa malipo ya banda moja)*

Kwa mantiki hiyo, tunapenda kuchukua fursa hii kukufahamisha rasmi na kukuomba kushiriki, pamoja na, kuiomba Ofisi yako isaidie kuhamasisha mitandao uliyonayo iii waweze kushiriki katika Maonyesho haya muhimu. Washiriki watahitajika kujaza Fomu ya Ushiriki iliyoambatishwa katika barua hii. Fomu hizi zinapatikana pia katika tovuti zifuatazo: www.awotta.org na www.twcc-tz.org. Mwisho wa kujaza fomu na kulipia ni tarehe 21st Januari 2019. *Punguzo la bei la asilimia 10 litatolewa kwa watakao/ipa kabla ya tarehe 30 Disemba 2018.*

Kwa mawasiliano zaidi, tafadhali wasiliana na wafuatao:

Mary Kalikawe +255 622 819 889 au mkalikawe@awotta.org
Kelly Kamala +255 693 456 104 au kkamala@awotta.org

Tunatanguliza shukrani za dhati kwa ushirikiano wako endelevu.

Wasalaam,

Mary Kalikawe
Chairperson - AWOTTA

UWANDAE EXPO2019
FOMU YA USAJILI

Aina	Ukubwa/	Gharama	Vitu vinavyotolewa
Platinum	3 x 6 sqm	TZS 800,000.00 + Ufadhili usiopungua Tshs 2.5 Milioni	Banda, meza, viti vitatu (bora), tiketi 5 za Cocktail ya Ufunguzi wa Maonyesho, nembo kuwekwa kwenye matangazo, kutangaza bidhaa kwenye documentary ya pili*
Premium	3 x 6 sqm	Tshs 800,000.00	Banda, meza, viti wiwili (bora), tiketi 3 za Cocktail ya Ufunguzi wa Maonyesho
Corporate	3 x 3 sqm	Tshs 500,000.00	Banda, meza, viti viwili, tiketi 1 ya Cocktail ya Ufunguzi wa Maonyesho
MSEs	2 x 3 sqm	Tshs 300,000.00	Banda, meza na viti viwili (watu wawili wanaweza kutumia banda moja kwa mkataba wa malipo ya banda moja)*

Fomu ya Usajili wa kuhudhuria Maonyesho kama Mdhamini / Mshiriki

Jina la Kampuni (Binafsi/Pamoja):	
Aina:	
Idadi ya Mabanda:	
Jina la anayeomba : Barua Pepe:	
Anuani ya Kampuni: Anuani ya Posta, Mji,	
Namba ya TIN: Namba ya VAT:	
Jina la Mhusika wa	
Simu ya Mkononi:	Barua Pepe:
Mahali, Tarehe:	Saini & Muhuri:

Kwa kusaini fomu hii ya usajili, unakubaliana na Masharti ya kushiriki/malipo na ya kusitisha ushiriki wako.

Ofa Maalum: Watakaowahi kulipa kabla ya tarehe 30 Disemba 2018 watapata 10% Punguzo la Bei.

MASHARTI YA MALIPO NA KUFUTA

Masharti ya Malipo:

Malipo yote yafanyike kwa fedha ya Shilingi ya kiTanzania.

Asilimia 50 ya jumla ya ada ya maonyesho yatadaiwa baada ya kupokea fomu ya usajili wa maonyesho kukamilika na kupokelewa kwa malipo kutathibitisha usajili. Malipo ya mwisho yanatakiwa kufanyika ifikapo tarehe **21 Januari 2019**.

Masharti ya Kufuta: Kuondolewa na mabadiliko ya usajili wako wa awali lazima ufanyike kwa maandishi: info@awotta.org na iwe kabla ya tarehe **20 Disemba 2018**.

Malipo ya Kufuta: 50% ya jumla ya ada ya maonyesho itarejeshwa iwapo umefuta kabla ya tarehe 20 **Disemba 2018**. Baki ya gharama ya maonyesho ya jumla ya 100% itachukuliwa baada ya tarehe hiyo.

TARATIBU NA MASHARTI KWA AJILI YA WADHAMINI NA WASHIRIKI

1. **Usajili wa Wadhamini na Washiriki**

Ili kuzingatiwa kama Mdhamini/au Mshiriki, fomu ya usajili inapaswa kukamilika, kusainiwa na kuwekwa mhuri kwa mtu aliyeidhinishwa na kupelekwa AWOTTA kabla ya tarehe ya mwisho. Katika hali ya kukubalika, Wadhamini/Washiriki watafungwa na Taratibu na Masharti ya Wadhamini na Washiriki.

AWOTTA ina haki ya kukataa usajili wowote kwa Mdhamini/Mshiriki bila kutoa sababu. Eneo la Maonyesho linatolewa kwa mujibu wa sera ya malipo na kufuta kama ilivyoorodheshwa hapo juu kwa Wadhamini na Washiriki. Kampuni yoyote ambayo haitii maagizo ya AWOTTA na washiriki wake inaweza kufutwa kutoka kwenye maonyesho. Makampuni hayo yanastahili kufanya malipo yote, na kwa gharama zote zinazojumuisha ikiwa ni pamoja na kodi yoyote ya thamani. Mikataba yote ya mdomo, ruhusa maalum na mipangilio maalum ni halali tu baada ya kupokea uthibitisho wa kimaandishi kutoka AWOTTA.

2. **Wajibu na Haki za Mshiriki**

Mabanda ya maonyesho yanaweza kutumiwa tu kwa kuonyesha na kutangaza bidhaa, vifaa au huduma za Mshiriki. Banda la SME's linaweza kutumiwa na watu wawili na wanapaswa kukubaliana jina ambalo litasajiliwa kwa kutaja sehemu ya kushiriki pamoja katika fomu ya usajili. Kutoa sehemu au kukodisha kwa kibinafsi kwa kibanda kwa mtu wa tatu, pamoja na makubaliano ya faragha kwa kubadili vibanda au nafasi ya sakafu kati ya washiriki wawili wa kujitegemea ni marufuku. AWOTTA ina haki ya kuingia ndani ya banda lolote wakati wowote. Mabanda na kumbi za maonesho yanapaswa kuwa wazi na kutumiwa wakati wote wa maonyesho. Ni kinyume cha sheria kwa makampuni, ambayo sio washiriki, kutangaza chochote kwa njia yoyote katika viwanja vya maonyesho au katika njia za kuingia kwenye viwanja hivi vya maonyesho.

3. **Wajibu na Haki za Mratibu**

AWOTTA ina haki ya kurekebisha wakati na eneo la maonyesho au kupunguza muda wa maonyesho. Mabadiliko yoyote kuhusu wakati na muda wa maonyesho hayataruhusu mdhamini/mshiriki kufuta mkataba wala kuomba kupunguziwa ada au kufanya madai ya uharibifu unaosababishwa na mabadiliko haya.

4. **Bima ya Madeni**

vyote vinavyowekwa na mshiriki havina bima ya AWOTTA au Makumbusho ya Taifa na hawatakuwa na madai yoyote kwa hasara yoyote, kuharibiwa au uharibifu utakaosababishwa kwa vifaa vyao, bidhaa au mali ya mshiriki. Washiriki wanakubali kuwajibika kwa mali zao na wafanyakazi wao, AWOTTA haitawajibika kwa majeruhi wowote katika wafanyakazi wa wafadhili/washiriki wanaohudhuria maonesho haya

5. Kuwekwa kwa mabanda ya maonyesho

Ili kuhakikisha uendeshaji mzuri wa UWANDAE EXPO 2019, Wadhamini/Washiriki wanapaswa kutii na kufuata maelekezo yote na mwongozo wa AWOTTA kuhusu matumizi ya mabanda, mapambo yao na vifaa vinavyofungwa ndani ya mabanda. Mabanda yatakuwa aina ya kawaida. Tofauti yoyote ya banda kutoka katika mwongozo huu, itahitaji idhini maalum ipatikane mapema kutoka AWOTTA. Ruhusa ya maandishi pia inahitaji kwa mabadiliko yoyote katika ukubwa au muundo wa nafasi ya sakafu, au kwa mabadiliko yoyote kwa vitu vingine vya ziada vya kukodishwa ambavyo vilipendekezwa na Mdhamini/Mshiriki.

6. Matengenezo ya mabanda na eneo la maonyesho

Wadhamini/Washiriki wanawajibika kwa uangalifu na usalama wa mabanda waliyopewa na vifaa vyake. Vibanda vilivyokodishwa na vifaa vya ndani lazima virejeshwe kwa hali iliyokubaliwa na kwa utaratibu sahihi. Ili kuepuka mikwaruzo na matundu kwenye sakafu kama matokeo ya kuburuza mizigo mizito ya chuma, washiriki wanatakiwa kutumia vifuniko vya kukinga kwa nje. Washiriki ambao wanataka kuonyesha vitu vizito ambavyo vinahitaji viegesho maalum au sakafu ni lazima kuomba idhini ya awali hasa katika suala hili kutoka AWOTTA. Haikuruhusiwi kugonga misumari au pini kwenye kuta za makumbuso ya taifa (eneo la maonesho), kuweka nyaya za umeme au kukata au kuchimba mashimo katika kuta za mabanda yaliyokodishwa bila kibali cha awali cha AWOTTA.

Hairuhusiwi sehemu yoyote ya banda la maonyesho kusimamishwa kutoka darini. Hairuhusiwi sehemu ya maonyesho au ya muundo wa banda kutumika zaidi ya eneo lililokodishwa kutoka upande wowote. Hakuna mabango yatakayoruhusiwa kuvuka zaidi ya kuta za kibanda husika. Vifaa vya kupamba na karatasi za ukutani zitakazotumiwa ni lazima ziwe za kudhibiti moto. Kabla ya kutumia vifaa hivyo, hakikisha umepata ruhusa kimaandishi kutoka AWOTTA. Kanuni za polisi, kanuni za zima moto na sheria nyingine zinapaswa kuzingatiwa wakati wote, ikiwa ni pamoja na wakati wa kuweka na kuondoa mabanda.

7. Kuwekwa kwa umeme/matumizi

Gharama zote zinazohusiana na nguvu kuu ya umeme wa mabanda na vifaa vya umeme vya mabanda zitabebwa na AWOTTA. Hata hivyo, AWOTTA haitawajibika na upotevu au uharibifu wowote, ambao unaweza kutokea kutokana na mapungufu kwenye mitambo ya umeme au kasoro yoyote kipindi chote cha Maonyesho.

8. Kuondolewa kwa vibanda

Mshiriki ni lazima aondoe vitu vyake katika eneo laibanda kwa gharama yake na AWOTTA haitahusika na vitu vitakavyosahaulika baada ya kufungwa kwa maonesho. Vitu vilivyokodishwa, vilivyokubaliwa awali kuwa vyema na mshiriki, vinapaswa kurejeshwa pasipo uharibifu wowote na vikiwa katika hali ya kuridhisha. Vitu vyote vya kukodisha vinachukuliwa kuwa katika hali ya kuridhisha isipokuwa pale ambapo AWOTTA inakuwa imetambua kitu kimaandishi wakati wa kukodisha. Washiriki watalazimika kubeba gharama za matengenezo au marekebisho ya maeneo ya maonyesho waliyoyaharibu. Vitu vyote vilivyokodishwa virudishwe katika hali ya usafi.

9. Malipo – uvunjaji wa mkataba

Tafadhali rejea masharti ya malipo, ofa maalum na masharti ya kufuta. Mkataba utabaki imara katika makubaliano ya AWOTTA na kampuni inayojisajili. Vipimo vya mabanda kwa kila aina yaliyotolewa kwa wastani ni kama ilivyoandikwa. AWOTTA ina haki ya kubadili vipimo hivi ili kutumia eneo kubwa zaidi la maonyesho. Bei zilizotolewa ni kulingana na vipimo halisi; ikiwa itajulikana baadaye kuwa nafasi ya ziada kweli imetumiwa kuliko ilivyoamriwa awali, ada stahili ya ziada itapaswa kulipwa mara moja. Maombi maalum kuhusu kuwekwa kwa mabanda yatapokelewa. Aidha, AWOTTA ina haki ya kupunguza kiasi cha nafasi ya sakafu iliyoombwa. Washiriki wanapaswa kubeba gharama za mitambo yoyote maalum watakayohitaji.

10. Sheria

Sheria itakayotuongoza itakuwa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.